For Educator Use Only SPECIAL EDUCATION and RELATED SERVICES (Kwa matumizi pekee ya mwalimu ELIMU MAALUMU na HUDUMA ZINAZOHUSIANA)

Utaratibu angalizi na taafira kwa Wazazi/Walezi

Ufuatao ni muhtasari mfupi wa baadhi ya haki za wanafunzi wenye ulemavu na wazazi wao. Tafadhali, rejea kijitabu cha *Utaratibu Angalizi Wa Kulinda Watoto Wenye Ulemavu Pamoja Na Wazazi* wao kwa kina na mapana yake katika maelezo.

USHIRIKI WA MAANA WA WAZAZI

- Wazazi wana haki ya kushiriki katika mikutano inayofanywa kwa kufuata utambulisho, tathmini, uwekaji wa wanafunzi wao kimasomo na utoaji wa elimu ya bure ya umma kama ilivyotajwa kwenye (elimu ya mtu binafsi, au elimu ya mtu mmoja mmoja) Individualized Education Program - IEP (EYMB ama EYMMM) . Wafanyakazi wa shule wanaweza kuwa na mikutano isiyo rasmi bila wazazi kuwepo.
- Tathmini za mwisho za huduma maalumu ya elimu zinafanywa kupitia utaratibu wa Individualized Education Program (elimu ya mtu binafsi, au elimu ya mtu mmoja mmoja IEP (EYMB ama EYMMM), na wazazi ni sehemu shirikishi na muhimu katika tahmini hiyo.
- Wazazi wana haki ya kupokea ripoti ya mara kwa mara kuhusu maendeleo ya watoto wao ndani ya malengo ya mpango wa Individualized Education Program (elimu ya mtu binafsi, au elimu ya mtu mmoja mmoja) IEP (EYMB ama EYMMM), kwa wakati ule ule ambao shule zinatoa kadi za ripoti kwa wanafunzi wote.

REKODI ZA ELIMU na USIRI

- Wazazi wanaweza kutizama rekodi za elimu maalumu ya wanafunzi wao. Rekodi hizi hutunzwa kwa siri katika faili iliyofungwa mbali, na kutengwa tofauti kabisa na rekodi za mara kwa mara za shuleni. Rekodi hizi haziwezi kutolewa au kufunguliwa kwa mtu yeyote yule bila ruhusa ya wazazi au walezi, isipokuwa kwa wafanyakazi wa wilaya wanaohusika na kushughulika na elimu ya mwanafunzi.
- Wazazi wana haki ya kuomba hizo habari kuhusu rekodi za watoto wao ziweze kurekebishwa kama wanaamini haziko sahihi au zinapotosha.
- Endapo wazazi wakiomba hizo habari, wapatiwe nakala za hizo rekodi ndani ya muda muafaka na mzuri.

IDHINI/RUHUSA

- Wazazi lazima wakubali, kwa maandishi, kabla ya tathmini ya mwanzo na hatua ya uwekaji wa watoto wao katika mfumo wa elimu maalumu.
- Idhini ya wazazi ni hiari, na inaweza kuondolewa muda wowote kwa kutumia maandishi yao.
- Ni sera ya Utah State Board of Education (Bodi ya Elimu jimbo la Utah), USBE (BYEJLU), kutuma rekodi za kielimu za mwanafunzi bila idhini ya wazazi au mwanafunzi mwenye umri mkubwa au tangazo fupi kwenda kwa viongozi wa shule nyingine au wilaya ambayo mwanafunzi anataka au anatarajia kujiunga.

TATHMINI HURU YA KIELIMU

- Wazazi wanaweza kuomba tathmini huru ya wanafunzi wao, ikiwa hawakubaliani na tathmini yote au sehemu Fulani ya tathmini iliyofanywa na timu ya shule husika. Mwalimu husika wa elimu maalumu anaweza kuwatuma wazazi kwa mkurugenzi wa wilaya kitengo cha elimu maalumu ili kujadili ombi lao na taratibu za kufuata.

NIDHAMU

- Haki za wanafunzi wenye ulemavu, kuhusu nidhamu, zinaambatana na sera salama za kishule za DSD's. Habari maalumu zinapatikana ndani ya kijitabu cha taratibu za kiulinzi kwa watoto wenye ulemavu na wazazi wao. *Procedural Safeguards for Children with Disabilities and Their Parents (Utaratibu Angalizi Wa Kulinda Watoto Wenye Ulemavu Pamoja Na Wazazi)*
- Wanafunzi wana haki ya kupata huduma sahihi na yenye kufaa katika elimu ya jumla na katika malengo ya IEP, ikiwa wametolewa shuleni ndani ya siku kumi za masomo kutokana na vitendo vya kinidhamu.

MCHAKATO WA MALALAMIKO

- DSD inataka kuhakikisha kwamba malalamiko ya wazazi kuhusu elimu maalumu ya wanafunzi wao yanashughulikiwa. Wasi wasi na malalamiko ya wazazi yanashughulikiwa kwa kufuata ngazi zifuatazo:
    1. Mkutano wa timu ya IEP
    2. Mwalimu mkuu (Building Principal)
    3. Msimamizi wa Wilaya (Huduma Za Elimu Maalumu) SPED
    4. Mkurugenzi, elimu maalumu
    5. Msimamizi mkuu wilaya (District Superintendent)
    6. USBE – Huduma Za Elimu Maalumu (SES)
- Kama malalamiko yasipotatuliwa, na wazazi wakahisi wilaya imekiuka masharti/mahitaji ya Individuals with Disabiliaties Education Act (Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu), IDEA (SYEYWWU)na wanataka kundika malalamiko rasmi, basi malalamiko hayo ni lazima yatumwe kwa msimamizi mkuu wa wilaya au kwa mkurugenzi wa elimu maalumu wa jimbo husika kitengo cha Utah State Board of Education (Bodi ya Elimu jimbo la Utah), USBE (BYEJLU), ambaye atachunguza yeye mwenyewe au atateua mtu mwingine kuchunguza malalamiko husika.
- Ikiwa wilaya haiwezi kutatua malalamiko, hatua za usuluhishi zitashauriwa au kufuatwa. Ikiwa usuluhishi haukufanikiwa, wazazi wanaweza kuomba kikao cha kusikilizwa. Hili ombi ni lazima liwe katika maandishi na kupelekwa kwa msimamizi wa wilaya (District Superintendent).

SHULE BINAFSI

- Davis School District (Wilaya ya shule ya Davis), DSD (WYSYD) inatakiwa kuwapa wazazi taarifa kwamba, udhamini wa kuwapeleka wanafunzi shule binafsi unapatikana kwa wanafunzi wenye ulemavu kupitia programu ya udhamini ya Carson Smith. Habari kuhusu udhamini huo zinapatikana kupitia tovuti ya USBE, https://www.schools.utah.gov/specialeducation/resources/scholarships
- Wazazi wana jukumu la kutoa taarifa ya maandishi kwenda kwa mkurugenzi wa wilaya kitengo cha elimu maalumu ndani ya siku 10 za kazi, **ikiwa wana nia ya kumuondoa mwanafunzi wao kutoka shule ya umma**, na kumuweka shule binafsi na wana nia ya kutaka marejesho ya malipo.

Kumbukizi kwa mwalimu: Unaposoma wakala huu, badili "mzazi" kwenda "mlezi au mwanafuzi mtu mzima" vile ipasavyo.